



Niliingia shule ya ufundi ya Don Bosko, - Don Bosco Boys Town Karen Nairobi 1990. Nilikutana na mapadre Waselesiani waliokuwa tofauti kabisa na mapadri wengine. Walikuwa wakarimu, marafiki, walimu. Hawa mapadre na Mabroda walishiriki kazi zetu, tulicheza pamoja nao, tulisali pamoja, walitufundisha darasani; walitupenda sana. Wakati wa mapumziko walikuwa pamoja nasi, na hata mara nyingi sana walikula chakula pamoja nasi. Tukiwa Karakana, walitembea kuona maendeleo

yetu, na pia walitusaidia kuelewa maarifa hapa na pale na kutupatia matumaini.

Mapadre Waselesiani pamoja na Mabroda walitupatia nafasi za purudani, michezo na mambo yanayofurahisha vijana. Kukaa Don Bosko kila mmoja aliweza kuelewa na kukuza talanta yake, katika michezo, muziki, uchoraji na pia katika utakatifu na elimu. Mara nyingi tukiwa wanafunzi, mapadre hao walitufundisha hasa kumhusu Mt. Yohane Bosko, Mt. Dominiko Savio na pia Maria Msaada wa Wakristo.

Mwaka 1992 nilienda Don Bosco Embu, shule ya sekondari na ufundi ya Waselesiani wa Don Bosko. Hapo kulikuwa na mapadre Wataliano ambaye waliokuwa wamebobeza katika muziki, ufundi, ukulima na elimu. Hao pia walinilea katika karama hiyo hiyo ya Mt. Yohane Bosko. Nyakati zote nilijisikia nyumbani. Ndivyo nilivutiwa na wito wa kuwa mmoja wao hadi sasa mimi ni padre Msalesiani. Ntoa shukrani zangu kwa Mungu kwa njia ya kuandaa kitabu hiki cha Maria Msaada wa Wakristo kwa ajili ya kueneza ibada hii ya Maria Msaada wa Wakristo na pia kukuza Karama ya Mt. Yohane Bosko ndani ya vijana. Baada ya kusomea na kulelewa katika shule na Seminari za Mt. Yohane Bosko najivunia kuwa Msalesiani wa Don Bosko. Ni wajibu wangu kupekua yaliyo ndani na kuwasaidia wengine kuelewa zaidi.

Pd. Paul Luseno Khanyonyi, SDB

Maria Msaada Wa Wakristu

Maria Msaada Wa Wakristu



Pd. Paul Luseno Khanyonyi, SDB